# The Lord Jesus Christ Will Come Again

By President Russell M. Nelson
*President of The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints*

# Bwana Yesu Kristo Atakuja Tena

Na Rais Russell M. Nelson
*Rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho*

October 2024 general conference

---

*Now is the time for you and for me to prepare for the Second Coming of our Lord and Savior, Jesus the Christ.*

My dear brothers and sisters, I am grateful that the Lord has blessed me to speak with you.

In this conference, the Lord has spoken to us through His servants. I urge you to study their messages. Use them as a litmus test of what is true and what is not during the next six months.

The preservation and renovation of the Salt Lake Temple and other areas on Temple Square have been underway for nearly five years. Present projections indicate that this work will be completed by the end of 2026. We are grateful for all who are working on this massive project.

During the last six months, we have dedicated or rededicated nine temples in five countries. Between now and the end of the year, we will dedicate five more.

Today we are pleased to announce plans to construct 17 more temples. Please listen reverently as I announce the locations.

Juchitán de Zaragoza, Mexico
Santa Ana, El Salvador
Medellín, Colombia
Santiago, Dominican Republic
Puerto Montt, Chile
Dublin, Ireland
Milan, Italy
Abuja, Nigeria
Kampala, Uganda
Maputo, Mozambique
Coeur d’Alene, Idaho

*Sasa ni wakati wako na mimi wa kujiandaa kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo.*

Wapendwa kaka na dada zangu, ninashukuru kwamba Bwana amenibariki kuzungumza nanyi.

Katika mkutano huu, Bwana amezungumza nasi kupitia watumishi Wake. Ninawaasa kujifunza jumbe zao. Zitumieni kama kipimo cha litmasi cha kipi ni kweli na kipi sicho kwa wakati wa miezi sita ijayo.

Utunzaji na uboreshaji wa Hekalu la Salt Lake na maeneo mengine ya Temple Square umekuwa ukiendelea kwa takribani miaka mitano. Matarajio ya sasa yanaonyesha kwamba kazi hii itamalizika mwishoni mwa 2026. Tunawashukuru wale wote wanaofanya kazi kwenye mradi huu mkubwa.

Wakati wa miezi sita iliyopita, tumeweka wakfu au kurudia kuweka wakfu mahekalu tisa katika nchi tano.Kati ya sasa na mwishoni mwa mwaka, tutaweka wakfu mengine ya ziada matano

Leo tunafurahia kutangaza mipango ya kujenga mahekalu 17 zaidi. Tafadhali sikilizeni kwa unyenyekevu wakati nikitangaza maeneo.

Juchitán de Zaragoza, Mexico
Santa Ana, El Salvador
Medellín, Colombia
Santiago, Dominican Republic
Puerto Montt, Chile
Dublin, Ireland
Milan, Italy
Abuja, Naijeria
Kampala, Uganda
Maputo, Msumbiji
Coeur d’Alene, Idaho

Queen Creek, Arizona
El Paso, Texas
Huntsville, Alabama
Milwaukee, Wisconsin
Summit, New Jersey
Price, Utah

My dear brothers and sisters, do you see what is happening right before our eyes? I pray that we will not miss the majesty of this moment! The Lord is indeed hastening His work.

Why are we building temples at such an unprecedented pace? Why? Because the Lord has instructed us to do so. The blessings of the temple help to gather Israel on both sides of the veil. These blessings also help to prepare a people who will help prepare the world for the Second Coming of the Lord!

As the prophet Isaiah prophesied, and as memorialized in Handel'sMessiah, when Jesus Christ returns, "the glory of the Lord shall be revealed, and all flesh shall see it together."

In that day "the government shall be upon his shoulder: and his name shall be called Wonderful, Counsellor, The mighty God, The everlasting Father, The Prince of Peace."

Jesus Christ will govern from both old Jerusalemand the New Jerusalem "built upon the American continent."From these two centers, He will direct the affairs of His Church.

In that day the Lord will be known as "King of Kings, and Lord of Lords." Those who are with Him will be "called, and chosen, and faithful."

Brothers and sisters, now is the time for you and for me to prepare for the Second Coming of our Lord and Savior, Jesus the Christ.Now is the time for us to make our discipleship our highest priority. In a world filled with dizzying distractions, how can we do this?

Regular worship in the temple will help us. In the house of the Lord, we focus on Jesus Christ. We learn of Him. We make covenants to follow Him. We come to know Him. As we keep our temple covenants, we gain greater access to the Lord's strengthening power. In the temple, we receive protection from the buffetings of the world. We experience the pure love of Jesus Christ and our Heavenly Father in great abundance! We feel peace and spiritual reassurance, in contrast to the turbulence of the world.

Queen Creek, Arizona
El Paso, Texas
Huntsville, Alabama
Milwaukee, Wisconsin
Summit, New Jersey
Price, Utah

Wapendwa kaka na dada zangu, je, mnaona kinachoendelea mbele ya macho yetu kwa sasa? Ninasali kwamba hatutakosa utukufu wa wakati huu! Bwana kwa hakika anaharakisha kazi Yake.

Je, kwa nini tunajenga mahekalu kwa kasi isiyo na kifani? Kwa nini? Kwa sababu Bwana ametuelekeza kufanya hivyo. Baraka za hekaluni husaidia kuikusanya Israeli pande zote mbili za pazia. Baraka hizi pia husaidia kuwaandaa watu ambao watasaidia kuandaa ulimwengu kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana!

Kama nabii Isaya alivyosema, na kama ilivyonukuliwa kwenye wimbo wa Handel waMessiah, wakati Yesu Kristo atakaporudi, "utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja."

Katika siku ile "uweza wa kifalme utakuwa begani mwake: Naye ataitwa jina lake Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani."

Yesu Kristo ataongoza kutoka kote Yerusalemu ya zamanina Yerusalemu Mpya "iliyojengwa kwenye bara ya Amerika."Kutoka vituo hivi viwili, ataendesha mambo ya Kanisa Lake.

Katika siku ile Bwana atajulikana kama "Mfalme wa Wafalme, na Bwana wa Mabwana." Wale ambao watukuwa Naye "wataitwa wateule, na waaminifu."

Akina Kaka na dada, sasa ni wakati wako na mimi wa kujiandaa kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo.Sasa ni wakati wa kufanya ufuasi wetu kuwa kitu cha kipaumbele. Katika ulimwengu uliojaa vivuruga mawazo vya kutia kizunguzungu, tunawezaje kufanya hili?

Kuabudu hekaluni mara kwa mara kutatusaidia. Katika nyumba ya Bwana, tunafokasi kwa Yesu Kristo. Tunajifunza kumhusu Yeye. Tunaweka maagano ya kumfuata Yeye. Tunakuja kumjua Yeye. Tushikapo maagano ya hekaluni, tunapata ufikiaji mkubwa wa nguvu ya Mungu ya kuimarisha. Hekaluni, tunapokea ulinzi dhidi ya majaribu ya ulimwengu. Tunapata uzoefu wa upendo msafi wa Yesu Kristo na Baba yetu wa Mbinguni kwa wingi. Tunahisi amani na uhakikisho wa kiroho, dhidi ya dhoruba za ulimwengu.

Here is my promise to you: Every sincere seeker of Jesus Christ will find Him in thetemple. You will feel His mercy. You will find answers to your most vexing questions. You will better comprehend the joy of His gospel.

Hii ni ahadi yangu kwenu: Kila anayemtafuta Yesu Kristo kwa dhati atampata hekaluni.Utahisi rehema Yake. Utapata majibu ya maswali yako magumu. Utaweza kuelewa zaidi shangwe ya injili Yake.

I have learned that the most crucial question we each must answer is this: To whom or to what will I give my life?

Nimejifunza kwamba swali la msingi zaidi ambalo kila mmoja wetu anatakiwa kulijibu ni hili: Ni kwa nani au kwa kipi nitayakabidhi maisha yangu?

My decision to follow Jesus Christ is the most important decision I have ever made. During medical school, I gained a testimony of the divinity of God the Father and His Son, Jesus Christ. Since then our Savior has been the rock upon which I have built my life.That choice has made all the difference! That decision has made so many other decisions easier. That decision has given me purpose and direction. It has also helped me weather the storms of life. Let me share two examples:

Uchaguzi wangu wa kumfuata Yesu Kristo ni wa muhimu zaidi ambao nimewahi kufanya. Wakati wa mafunzo yangu ya udaktari, nilipata ushuhuda wa utakatifu wa Mungu Baba na Mwanawe, Yesu Kristo. Tangu hapo Mwokozi wetu amekuwa mwamba ambao juu yake nimejenga maisha yangu.Uchaguzi huo ulileta utofauti kwenye yote! Uchaguzi huo umewezesha chaguzi zingine nyingi kuwa rahisi sana. Uchaguzi huo umenipa dhumuni na mwongozo. Pia umenisaidia kukabiliana na tufani za maisha. Acha nishiriki mifano miwili:

First, when my wife Dantzel unexpectedly passed away, I could not reach any of our children. There I was, alone, devastated, and crying out for help. Gratefully, through His Spirit, the Lord taught me why my dear Dantzel had been taken home. With that understanding, I was comforted. Over time, I was better able to cope with my grief. Later, I married my beloved wife Wendy. She was a central part of my second example.

Kwanza, wakati Dantzel mke wangu alipofariki ghafla, sikuweza kumfikia mtoto wetu yoyote. Nilikuwa peke yangu, niliyekata tamaa na mwenye kulia kwa ajili ya msaada. Nashukuru, kupitia Roho Wake, Bwana alinifundisha sababu ya kwa nini Dantzel alikuwa amerudishwa nyumbani. Kwa uelewa huo, nilipata faraja. Kadiri muda ulivyoenda, niliweza kuzoea huzuni yangu. Baadaye, nilimuoa Wendy mke wangu mpendwa. Yeye alikuwa kitovu cha mfano wangu wa pili.

When Wendy and I were on assignment in a distant land, armed robbers put a gun to my head and pulled the trigger. But the gun did not fire. Throughout that experience, both of our lives were threatened. Yet Wendy and I felt an undeniable peace. It was the peace “which passeth all understanding.”

Wakati Wendy pamoja nami tukiwa kwenye jukumu katika nchi ya mbali, wanyang’anyi wenye silaha waliweka bunduki kichwani kwangu ili kunipiga risasi. Lakini risasi haikutoka. Katika uzoefu huo, maisha yetu wote wawili yalikuwa yametishwa. Hata hivyo, Wendy na mimi tulihisi amani isiyozuilika. Ilikuwa ni amani “ipitayo akili zote.”

Brothers and sisters, the Lord will comfort you too! He will strengthen you. He will bless you with peace, even amidst chaos.

Akina kaka na dada, Bwana atawafariji ninyi pia! Yeye atawaimarisha. Yeye aawabariki kwa amani, hata katikati ya machafuko.

Please listen to this promise of Jesus Christ to you: “I will be on your right hand and on your left, and my Spirit shall be in your hearts, and mine angels round about you, to bear you up.”

Tafadhali sikilizeni ahadi hii ya Yesu Kristo kwenu: “Nitakuwa mkono wenu wa kuume na wa kushoto, na Roho wangu atakuwa mioyoni mwenu, na malaika wangu watawazingira, ili kuwabeba juu.”

There is no limit to the Savior’s capacity to help you. His incomprehensible suffering in Gethsemane and on Calvary was for you! His infinite Atonement is for you!

Uwezo wa kuwasaidia wa Mwokozi hauna ukomo. Mateso yake yasiyoelezeka huko Gethsemane na Kalvari yalikuwa kwa ajili yenu! Upatanisho Wake usio na mwisho ni kwa ajili yenu!

I urge you to devote time each week—for the

Ninawasihi kutenga muda kila wiki—katika

rest of your life—to increase your understanding of the Atonement of Jesus Christ. My heart aches for those who are mired in sin and don't know how to get out. I weep for those who struggle spiritually or who carry heavy burdens alone because they do not understand what Jesus Christ did for them.

Jesus Christ took upon Himselfyoursins,yourpains,yourheartaches, andyourinfirmities.You do not have to bear them alone! He will forgive you as you repent. He will bless you with what you need.He will heal your wounded soul.As you yoke yourself to Him, your burdens will feel lighter.If you will make and keep covenants to follow Jesus Christ, you will find that the painful moments of your life are temporary. Your afflictions will be "swallowed up in the joy of Christ."

It is neither too early nor too late for you to become a devout disciple of Jesus Christ. Then you will experience fully the blessings of His Atonement. You will also be more effective in helping to gather Israel.

My dear brothers and sisters, in a coming day, Jesus Christ will return to the earth as the millennial Messiah. So today I call upon you to rededicate your lives to Jesus Christ. I call upon you to help gather scattered Israel and to prepare the world for the Second Coming of the Lord. I call upon you to talk of Christ, testify of Christ, have faith in Christ, and rejoice in Christ!

Come unto Christ and "offer your whole [soul]" to Him.This is the secret to a life of joy!

The best is yet to come, my dear brothers and sisters, because the Savior is coming again! The best is yet to come because the Lord is hastening His work. The best is yet to come as we fully turn our hearts and our lives to Jesus Christ.

I bear my solemn witness that Jesus Christ is the Son of God. I am His disciple. I am honored to be His servant. At His Second Coming, "the glory of the Lord shall be revealed, and all flesh shall see it together." That day will be filled with joy for the righteous!

Through the power of the sacred priesthood keys I hold, I declare this truth to you and to all the world! In the name of Jesus Christ, amen.

maisha yenu yote—kuongeza uelewa wenu wa Upatanisho wa Yesu Kristo. Moyo wangu hupata huzuni kwa ajili ya wale ambao wamekwama dhambini na hawajui namna ya kutoka. Ninahuzunika kwa ajili ya wale ambao wanahangaika kiroho au ambao wanabeba mizigo mizito wao wenyewe kwa sababu hawaelewi Yesu Kristo alifanya nini kwa ajili yao.

Yesu Kristo alijichukulia mwenyewe dhambizako,matesoyako,kuvunjika moyokwako,na magonjwayako.Huna haja ya kuyabeba mwenyewe! Yeye atakusamehe unapotubu. Yeye atakubariki na kile unachohitaji.Yeye atatibu nafsi yako iliyojeruhiwa.Unapojifunga nira pamoja Naye, mzigo wako utakuwa mwepesiKama utafanya na kushika maagano ya kumfuata Yesu Kristo, utagundua kwamba nyakati za maumivu za maisha yako ni za muda. Mateso yako "yatamezwa kwenye shangwe ya Kristo."

Si mapema wala muda haujapita wa wewe kuwa mfuasi wa kweli wa Yesu Kristo. Kisha utapata uzoefu mkamilifu wa baraka za Upatanisho Wake. Pia utakuwa na ufanisi zaidi katika kusaidia kuikusanya Israeli.

Kaka na dada zangu wapendwa, katika siku ijayo, Yesu Kristo atarudi duniani kama Masiya wa milenia. Hivyo leo ninawaasa kuweka wakfu tena maisha yenu kwa Yesu Kristo. Ninawaasa kusaidia kuikusanya Israeli iliyotawanyika na kuuandaa ulimwengu kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana. Ninawaasa kuongea kuhusu Kristo, kushuhudia kuhusu Kristo, kuwa na imani katika Kristo na kufurahia katika Kristo!

Njoo kwa Kristo na "jitoe [nafsi] yako yote" Kwake.Hii ndio siri ya shangwe maishani!

Mazuri bado yako njiani, kaka na dada zangu, kwa sababu Mwokozi anakuja tena! Mazuri bado yako njiani kwa sababu Bwana anaharakisha kazi Yake. Mazuri bado yako njiani wakati tunapogeuza mioyo na maisha yetu yote kwa Kristo.

Ninatoa ushahidi wangu wa dhati kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Mimi ni mfuasi Wake. Ninashukuru kuwa mtumishi Wake. Kwenye Ujio Wake wa Pili, "utukufu wa Bwana utafunuliwa na kila mwili utauona." Siku hiyo itajawa na shangwe kwa wenye haki!

Kupitia nguvu za funguo takatifu za ukuhani nilizonazo, ninatamka ukweli huu kwenu na kwa ulimwengu wote! Katika jina la Yesu Kristo, amina.